HUMAN DEVELOPMENT INNOVATION FUND

Funded by UKaid from the British people

TUME YA TAIFA YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Wito wa Fursa ya Kukuza Ubunifu Wako, 2018

1 Utangulizi

Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) na Mfuko wa Ubunifu wa Maendeleo ya Watu (HDIF) wanatoa wito wa mwaka 2018 wa maombi ya ***"Fursa ya Kukuza Ubunifu Wako".*** COSTECH na HDIF wanashirikiana kutoa fedha kwa mawazo yenye ubunifu kutoka kwa wananchi na taasisi za kitanzania kupitia wito wa ushindani wa maandiko ya miradi ya ubunifu. Mpango huu unafadhiliwa pia kwa kushirikiana na Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DFID). Lengo la wito huu ni kuimarisha mfumo wa ubunifu nchini Tanzania kupitia kujenga uwezo wa kubuni kwa watafiti, wajasiriamali binafsi, wabunifu kwa ujumla na wengineo.

2 Dhumuni

Kusudio la Mfuko wa Ubunifu ni kutoa msaada wa kifedha katika kuendeleza bunifu ambayo itachangia maendeleo ya kiuchumi na kijamii hapa Tanzania. Hii itatoa msaada wa kifedha kwa makampuni na jumuiya ya watafiti kwa kuchangia kuendelezwa kwa teknolojia na ubunifu hapa Tanzania. Ruzuku hii ni rasilimali chache kwa shughuli zilizo kubaliwa tu na zenye kuleta matokea yaliyo wazi na thabiti.

3 Wigo wa Mfuko

Mfuko huu wa ubunifu unalenga aina zote za ubunifu kwa kutoa motisha kwa ushirikiano baina ya watafiti na wagunduzi nje ya mfumo rasmi wa utafiti. Mfuko una lengo la kuziba pengo la kugharamia michakato ya ubunifu na kuwasaidia wabunifu kushirikiana na taasisi za umma, wajasiriamali binafsi na wadau wengine muhimu kama vile wazalishaji na watoa huduma.

4 Tarehe ya Kuanza: 09 Agosti 2018.

5 Tarehe ya Mwisho ya Kupokea Maombi: 08 Septemba 2018; Muda: 15:00 (Saa tisa mchana).

6 Muombaji / Waombaji

Mfuko huo utatolewa ili kusaidia ubunifu kutoka kwa makundi matatu kama yafuatayo:

i. Ubunifu kutoka kwa Watafiti

ii. Ubunifu kutoka kwa wabunifu/wavumbuzi katika makampuni ya biashara na taasisi/mashirika. Pia mbunifu binafsi
iii. Ubunifu wa kimaendeleo wa pamoja kati ya watafiti na wajasiriamali.

7 Aina ya Mifumo ya Ruzuku

7.2 **Uendelezaji**/*Ukuzaji wa Bidhaa (Teknolojia) za Mfano* (Prototype development)

Lengo la mpango huu wa kifedha ni kusaidia mwombaji au mbunifu kuendeleza utafiti wao na matokeo ya teknolojia ili kuendeleza zaidi mifano ya bidhaa/teknolojia hizo, kuanzisha/kufanikisha dhana ya wazo na uthibitisho wa masuala ya kibiashara

7.3 **Uendelezaji** *wa Teknolojia* (Technogical Development)

Mfuko huu unasaidia wabunifu kuendeleza teknolojia pamoja na mnyororo wa thamani wa ubunifu, kutoka kwenye ushahidi wa dhana (wazo) / mfano mpaka kuonyeshwa kwa teknolojia. Mtazamo ni juu ya shughuli zitakazoleta na kufanya ukuzaji na uendelezaji wa teknolojia wa awali/mwanzo kuvutia zaidi na kupunguza changamoto za masoko.

7.4 Ubiasharishaji (Commercialization Support Fund)

Mpango huu wa kifedha umeundwa kusaidia kujaribu kupima na kuthibitisha soko la kubiarashisha teknolojia au matokeo ya tafiti. Kusudi ni kuunganisha wabunifu wa teknolojia na fursa za biashara pamoja na fursa za uwekezaji.

8 Maeneo ambayo yataombewa fedha na kufadhiliwa

8.1 Uendelezaji/Ukuzaji wa Bidhaa (Teknolojia) za Mfano

a) Kuendeleza suluhu ndogo inavyowezekana (Development of minimal viable solution)
b) Kulinda haki miliki idhini (Protecting Intellectual Property (IP))
c) Majaribio ya kukubalika na watumiaji kwa bidhaa (User Acceptance Test)
d) Kuhakiki wazo la kibunifu/Utafiti wa awali wa masoko (Validation of Idea/Primary Market Research)

8.2 Uendelezaji wa Teknolojia

a) Kuendeleza suluhisho la mwisho (Development of the final solution)
b) Kuonyesha na kufanya majaribio ya teknolojia (Demonstration and piloting solution)
c) Support for certification activities
d) Protection Intellectual Property (IP)

8.3 Ubiasharishaji

a) Kupata vyeti na leseni husika (Acquiring required approved certification and licenses)
b) Mpango wa biashara (Business Plan development)

c) Shughuli za uendelezaji na masoko (Promotion and Marketing activities)
d) Kukuza bidhaa za mfano kuwa halisia (Up scaling)
e) Utawala wa mikataba (Contract management)
f) Utawala wa Haki Miliki Idhini (IP management).

9 VIGEZO VYA TATHMINI

Maombi yote yatatathminiwa dhidi ya vigezo vifuatavyo:-

9.1 Ubunifu

i. Upya wa bidhaa, huduma au mfano wa biashara nchini Tanzania AU uboreshaji wa umuhimu kwenye bidhaa, huduma au mfano wa biashara.
ii. Upya wa njia ya kufanya bidhaa zilizopo au huduma zinapatikana kwa walengwa
iii. Ushindani wa bidhaa au huduma katika soko

9.2 Uwezo

i. Uwezeshaji wa suluhisho kwa mlengwa mtumiaji wa mwisho
ii. Uendelevu wa mradi zaidi/baada ya kipindi cha msaada wa kifedha wa mfuko huu
iii. Uhalisia wa ufanisi wa ubunifu huo

9.3 Matokeo

i. Matokeo ya kijamii yanayotarajiwa/lengwa kufikiwa kupitia mradi huo.
ii. Jinsi mradi huo utavyopunguza athari mbaya/ matokeo hasi.

9.4 Ufanisi wa Timu

Timu inaweza kuwa mtu binafsi au kikundi cha watu.

i. Uwepo na upatikanaji wa uwezo/ustadi muhimu
ii. Msimamo thabiti wa wanachama/timu katika mradi huo wa ubunifu.

9.5 Ubiasharishaji na Ushindani wa Maombi

i. Je! ubunifu una uwezo wa ubiasharishaji/ kibiashara?
ii. Ushindani wa ubunifu

10 Muda wa Ruzuku: Hadi miezi 12 (2018-2019)

11 Kiasi cha Ruzuku kwa kila Mradi: Kiwango cha juu cha TZS 40,000,000. Kiasi cha miradi 15 itakayopita mchujo itapewa fedha. Kati ya hiyo: Miradi minne (4) itatoka kwa watafiti; Miradi minne (4) itatoka kwa wabunifu wa makampuni; na Miradi saba (7) itatoka kwa miradi ya ushirikiano wa watafiti na wajasiriamali.

12 UTARATIBU WA MAOMBI

12.1 Ni muhimu kwamba maombi yawasilishwe kupitia akaunti ya barua pepe ya Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (Tume) itakayotolewa na kupendekezwa na Tume; na

Wakuu/Viongozi wa Mradi huo lazima waonyeshe kiwango cha fedha zinazoombwa. Mapendekezo ya Maombi yaliyokamilika lazima yawasilishwe kwa Tume kupitia barua pepe hii: **innovationfund@costech.or.tz**

KUMBUKA: Barua pepe hizi ni kwa kuwasilisha Maombi ya Mapendekezo ya Mradi tu.

12.2 Maombi lazima yajumuishe: nakala kamili za fomu za maombi zilizojazwa kikamilifu, sehemu zote muhimu zilizobainishwa katika fomu za maombi lazima zijazwe ipasavyo na kiukamilifu. Fomu za maombi zisizokamilishwa hazitafanyiwa tathmini. Maombi yatakayofika/kutumwa baada ya tarehe ya mwisho/ kufunga kupokea maombi/mapendekezo hazitashughulikiwa. Fomu za maombi zinapatikana katika Tovuti ya Tume: www.costech.or.tz

12.3 Bajeti ya mradi haipaswi kuzidi kiasi kilichoelekezwa kwa kila mradi katika vigezo vya uwekezaji kama ilivyobainishwa katika aya ya 10 hapo juu; na

12.4 Mwombaji anapaswa kuwa na taasisi au asasi ambayo itamsimamia na atatakiwa kuambatanisha barua kutoka taasisi au asasi hiyo.

13 KUZINGATIA JINSIA

Uzingatizi wa jinsia ni miongoni mwa mambo ambayo lazima yazingatiwe katika uundaji wa timu/kikundi na utekelezaji wa mradi huo. Kwa hivyo, pendekezo la mradi lazima lionyeshe jinsi litakuwa na matokeo kwa wanaume na wanawake, na pia kuonyesha hatua ya kimkakati ya kuhusisha jinsia yenye kipaumbele hafifu.

14 LUGHA

Maombi yanaweza kufanywa kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza.

15 MAULIZO NA FOMU YA MAOMBI YA FEDHA/ RUZUKU

Ili kupata fomu ya maombi ya fedha/ Ruzuku na kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana kupitia kiunganishi kifuatacho hapa chini: https://goo.gl/forms/rSVQyTm27cJTpX2X2. Fomu ya maombi zinaweza kupatikana pia kwenye tovuti ya tume: www.costech.or.tz.